Sikika

Jarida la Sikika

Namba ya Usajili - 00005809 Toleo 7: Septemba, 2012

Huduma bora za afya kwa watanzania wote

Utangulizi

Na Thomas Ludovick

KARIBU katika jarida la Sikika **toleo la 7** lenye lengo la kukufahamisha baadhi ya shughuli za utetezi zilizotekelezwa ndani na nje ya shirika letu katika robo ya mwaka.

Shirika lilifanikiwa kufanya ufuatiliaji kuhusiana na *CT Scan* katika hospitali ya taifa ya Muhimbili (MNH), ambayo ilikuwa imeharibika kwa takriban miezi saba na kusababisha usumbufu m kubwa kwa wagonjwa.

Baadhi ya wajumbe wa Timu ya SAM Iramba wakichukua taarifa kutoka kwenye moja ya zahanati wilayani humo.

Katika kufuatilia, Sikika ilibaini kwamba takriban asilimia 6 ya wagonjwa (watu 1, 226) hufa kwa mwaka kutokana na ukosefu wa huduma za *CT Scan,* huku asilimia 90 ya wahanga wa ajali zinazotokea nchini wakishindwa kupata huduma hiyo.

Katika kuunga mkono juhudi za serikali za kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima tangu mwaka 2009/10, Sikika imekuwa ikifanya ufuatiliaji na uchambuzi wa taarifa katika baadhi posho zinazotolewa, mathalan za; mafunzo, usafiri, huduma za ukarimu, ununuzi wa magari na mafuta ya magari, Mafuta na vilainishi. Sikika tunaamini kwamba posho za aina hiyo si za lazima na kwamba fedha hizo zingeelekezwa kwenye matumizi muhimu kama vile kwenye kuboresha mazingira ya kazi, rasilimali watu, dawa na vifaa tiba.

Sikika pia ilitoa tamko la kulaani usambazaji wa dawa za kupunguza makali ya virusi vya ukimwi (ARVs), ambazo zilisababisha baadhi ya watu Wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (WAVIU) kuingiwa na hofu na kuanza kutupa au kusitisha matumizi ya dawa hizo na hivyo kuathiri afya zao. Kama sehemu ya kukabiliana na sakata hilo, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii iliamua kukifungia kiwanda kinachozalisha dawa hizo cha *Tanzania Pharmaceutical Industries Limited* (TPI), kwa uchunguzi zaidi.

Katika kipindi cha mwisho wa mwaka, shirika pia liliungana na watanzania wengine katika mchakato wa kuandaa maoni ya Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Tumeendelea kufanya kazi za utetezi juu utawala bora katika sekta ya afya kupitia vyombo mbalimbali vya habari nchini na kupitia mitandao ya *Twitter: (@sikika1), Facebook: (Sikika Tanzania)* na *Blog: www.sikika-tz.blogspot.com* katika kukuza mijada mbalimbali inayohusu bajeti, rasilimali watu, uwepo na upatikanaji wa dawa na vifaa tiba, UKIMWI/VVU na uwajibikaji kwa ujumla katika sekta ya afya.

Kwa taarifa zaidi tembelea tovuti yetu *www.sikika.or.tz* na kwa maoni tafadhali tutumie barua pepe kwenda *info@sikika.or.tz* au ujumbe mfupi wa maneno kupitia namba *0688 493 882.*

Ndani

CT Scan - kifaa muhimu kisichopewa umuhimu..... 1
Serikali ipunguze matumizi yasiyo na tija..... 2
ARVs bandia: Wizara iwatoe hofu watumiaji..... 3
Katiba ilinde afya za watanzania..... 4

Haliuzwi

CT Scan - kifaa muhimu kisichopewa umuhimu

Na Mwandishi Wetu

TAKRIBAN asilimia 6 ya wagonjwa (au watu 1,226) hufa kwa mwaka kutokana na ukosefu wa huduma ya CT Scan, huku asilimia 90 ya wahanga wa ajali zinazotokea nchini hushindwa kupata huduma hiyo.

Mashine ya CT Scan ambayo hutumika kusoma viungo ndani ya mwili wa binadamu katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), imekuwa ikiharibika kwa kipindi cha miezi saba na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wagonjwa.

Mashine ya CT Scan kifaa muhimu ambacho hutumika kusoma viungo ndani ya mwili wa binadamu.Picha kwa hisani ya mtandao.

Ufuatiliaji mdogo uliofanywa na Sikika umebaini kuwa mashine hiyo imeharibika tangu mwezi Novemba 2011 hadi mapema Juni, 2012. Uchunguzi huo ulifanyika kwa njia ya mapitio ya maandiko na mahojiano na watu kutoka taasisi za umma na binafsi zinazotoa huduma za CT Scan.

Mapitio ya maandiko yamebaini kuwa kuna idadi ndogo ya watumiaji wa CT Scan katika Tanzania ni mdogo kutokana na matengenezo ya mara kwa mara, kutozingatia ubora na ukosefu wa wataalamu wa kutosha.

Uchungu huo pia umebaini kuwa mahitaji ya matumizi ya CT Scan kwa nchi nzima ni 20,440 wanaohitaji huduma hiyo kwa mwaka, huku watu 56 wakihitaji huduma hiyo kwa siku.

Gharama ya kupata huduma ya CT Scan katika hospitali ya taifa Muhimbili ni TSh 170,000 wakati katika hospitali binafsi ni kati ya Tsh 150,000 hadi 500,000 kulingana na muda wa matumizi ya Scan na hospitali husika.

Hata hivyo, baadhi ya Madaktari wa hospitali ya taifa Muhimbili, walikuwa na maoni kwamba fedha zinazokusanywa wakati CT Scan ikiwa inafanya kazi zilikuwa si tu hazitoshi kulipia moja kwa moja gharama za kuendeshea CT Scan lakini pia kuwezesha ununuzi wa kifaa hicho kipya na kupunguza mzigo wa kazi ya CT Scan moja iliyopo sasa.

Mwezi mmoja baada ya utafiti mdogo uliofanywa na Sikika juu ya utetezi wa suala hilo, gazeti la ndani (Nipashe Agosti, 2012) liliripoti kuwa CT Scan katika hospitali ya taifa Muhimbili ilikuwa imeanza kutoa huduma.

Sikika inapendekeza kwamba kuwe na mipango wazi ya fedha na mikataba wakati wa ununuzi wa vifaa muhimu vya matibabu ili kuwe na muda maalumu wa matengenezo na kuongeza muda wa vifaa muhimu katika kufanya kazi. Pia Serikali kuu na serikali za mitaa zinahitajika kuhakikisha kuwa hospitali zote zina vifaa tiba muhimu vya afya, ambavyo vitasaidia katika kupunguza mateso na vifo visivyo vya lazima kwa raia.

Serikali ipunguze matumizi yasiyo na tija

Na Eva Emmanuel

MWANZONI mwa mwaka 2012, mgomo wa madaktari ulisababisha kuzorota kwa utoaji wa huduma za afya katika vituo vya umma, hivyo kusababisha mateso na athari za kiafya kwa baadhi ya wananchi. Mgomo huo wa aina yake uliibua hisia na changamoto nyingi zaidi hasa baada ya serikali kushindwa kukutana na madaktari ili kujadili nyongeza ya mishahara na kuboresha mazingira ya kazi kwa maelezo ya kutokuwa na fedha.

Tangu miaka 2009/10, Sikika imekuwa ikifuatilia utekelezaji wa sera ya Serikali ya kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima. Ni katika kuamini kwamba rasilimali za nchi zikitumika ipasavyo zitasaidia kuondoa hali duni na migomo inayoikumba sekta ya afya.

Kwa mantiki hiyo, tumefanya uchambuzi na kuainisha orodha ya kasma 6 katika bajeti ambazo matumizi yake yanahofiwa kutoleta tija katika ustawi wa jamii. Kasma hizo zinajumuisha aina zote za posho; mafunzo, usafiri, huduma za ukarimu, ununuzi wa magari na mafuta ya magari na vilainishi. Hatusemi kwamba mgawanyo wote huo sio wa lazima, kwani baadhi ya shughuli kati

Wanarakati wakiandamana na mabango kwenye makutano ya barabara za Ocean na Ali Hassan Mwinyi jijini Dar es Salaam kwa lengo la kushinikiza Serikali isikilize madai ya madaktari ili kumaliza mgomo wao.

ya hizo zina umuhimu mkubwa. Kinachohitajika ni uwazi katika kupanga bajeti na utekelezaji wa mchakato ili kutofautisha matumizi muhimu na yale yasiyo ya lazima.

Uchambuzi wa bajeti kwa miaka iliyopita unaonyesha kuwa mgawo katika orodha hiyo ya matumizi yasiyo ya lazima haujawahi kupunguzwa na badala yake umekuwa ukiongezeka. Mwaka 2009/10, jumla kuu ilikuwa ni Tsh. bilioni 535, mwaka 2010/11 ilikuwa Tsh. bilioni. 545 na kwa mwaka 2011/12, mgawo huo uliongezeka hadi kufikia Tsh. bilioni 558.

Zipo dosari mbalimbali katika maandalizi ya bajeti na mfumo wa usimamizi ambazo zinachangia katika kueleza ni kwa nini serikali inakwama kutekeleza sera yake ya kudhibiti matumizi ya fedha za umma. Moja ya eneo lenye tatizo tulilobaini ni lile la kutofautiana kwa gharama za kasma kwenye bajeti.

Ushahidi kutoka kwenye Mpango wa Matumizi wa Muda wa kati (MTEF) wa mwaka 2011/12-2013/14 wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii unaonyesha kwamba baadhi ya viwango vya kasma havikufuatwa ipasavyo. Wizara ilitumia viwango na gharama tofauti kwa kasma zinazofanana. Kwa mfano, bidhaa za *'chakula na vinywaji'* vipimo vilivyotumika ni ama kwa 'siku' au kwa 'mtu mmoja'. Kwa vipimo vya *'mafuta ya diesel*, wizara ilitumia viwango vya vipimo vya lita au 'robo mwaka'. Aidha, viwango vya gharama za vipimo vya *'vyakula na vinywaji kwa mtu'* vinatofautiana kati ya Tsh 20,000 na 1,920,000. Vile vile, bei ya 'Diesel kwa lita' ni kati ya Tsh. 1,500/- hadi 4,000/-.

Upangaji holela wa gharama za kasma hizi unasababisha bajeti kubwa isiyo ya lazima, ambayo ingeweza kutumika kusomesha madaktari au kununua madawa na vifaa tiba muhimu na vitanda hospitalini.

Sikika inapendekeza kwamba, ili kuimarisha mfumo wa utawala ambao unahusika na mchakato wa bajeti, Afisa masurufu na Kamati ya Bajeti wafuate viwango vya mipango ya bajeti na taratibu za mipango ya Serikali na waanzishe viwango sawa kwa kasma zote na kuandaa orodha ya bei za kasma mapema. Taarifa hizi pia ziwekwe wazi kwa wananchi ili kukuza uwazi wa bajeti.

ARVs bandia: Wizara iwatoe hofu watumiaji

Na Aisha Hamisi

TAARIFA za kusambazwa kwa dawa za kupunguza makali ya Virusi vya Ukimwi (ARV's) ambazo ni bandia, zimejenga hofu miongoni mwa wananchi wanaoishi na virusi vya Ukimwi (WAVIU) na kusababisha wengine ama kutupa dawa zao au kuacha kuzitumia kabisa.

Kutokana na hali hiyo, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilichukua uamuzi wa kukifungia kiwanda kinachozalisha dawa hizo cha *Tanzania Pharmaceutical Industries Limited (TPI).* Wizara pia ilisimamisha matumizi ya dawa hizo na kurudisha MSD zile ambazo zilikuwa kwenye vituo vya kutolea huduma.

Mmmoja wa maafisa kutoka Mamlaka ya Chakula na Dawa Nchini (TFDA) ambaye hakutaka jina lake liandikwe kwenye vyombo vya habari akiwaonesha waandishi wa habari Dawa badia za kupunguza makali ya Ukimwi (ARVs) zilizoondolewa katika vituo vya kutolea huduma mara baada ya kugundulika. Picha na Aron Msigwa – MAELEZO kwa hisani ya mtandao wa Thehabari.

Tunaipongeza Wizara kwa kuchukua hatua hizo lakini taarifa iliyotolewa na Waziri Dk. Hussein Mwinyi iliacha maswali kadhaa. Je, zoezi na kukusanya dawa hizo limekusanya pia zile ambazo tayari zilikuwa mikononi mwa watumiaji? Baadhi ya watumiaji huwa na kiasi kikubwa cha dawa majumbani kama tahadhari pindi zinapokosekana vituoni. Je, serikali imewafikia wote na kuwapa elimu, kuwaomba msamaha na kuwapatia ushauri wa kisaikolojia?

Ilielezwa pia kwamba Wizara imehakikisha ARVs zinazokidhi ubora zinaendelea kupatikana katika vituo vya kutolea huduma za afya kote nchini. Kwa kuwa dawa hizi zilikuwa zikizalishwa na kiwanda cha TPI pekee hapa nchini; je, Wizara imepata wapi hizo dawa mbadala? Ziliagizwa lini na ni kiasi gani? Zilifika na zilisambazwa vituoni lini?

Sikika inaishauri Wizara kufafanua na kutoa maelezo ya kina kwa wananchi ili kuwatoa hofu na kurejesha imani kwa watumiaji wa dawa hizo. Vilevile, tungependa kusikia kauli ya serikali kuhusu fidia kwa wale ambao tayari walitumia dawa hizo, iwapo watapata madhara yoyote kwa njia ya usugu, mlipuko wa magonjwa nyemelezi au vifo.

Taarifa za dawa na vifaa tiba bandia zimekuwa zikitolewa na watoa huduma kwa muda mrefu sasa. Itakuwa na tija zaidi kama uchunguzi wa ARV bandia utafanyika sambamba na kuchunguza aina nyingine za dawa na vifaa tiba ili kutatua tatizo la dawa zote zinazohisiwa kuwa za bandia. Tunashauri uwepo mfumo makini ambao utahakikisha hakuna dawa au vifaa tiba vinavyosambazwa kwa watumiaji kabla ya ukaguzi na uhakiki wa ubora wake.

Katiba ilinde afya za watanzania

Na Mwandishi Wetu

ILI kuimarisha sekta ya afya nchini na kulinda afya za wananchi, Sikika imependekeza katiba mpya itambue haki ya afya na kuipa ulinzi wa kutosha.

Maoni hayo yalitolewa hivi karibuni na Mwanasheria na Afisa Haki Afya wa Sikika, Bi. Geline Fuko katika mkutano wa vijana kutoka katika shule za sekondari na vyuo vikuu nchini. Afisa huyo alikuwa akitoa mada kuhusu wajibu wa katiba katika kuimarisha sekta ya afya nchini Tanzania.

Mwanasheria na Afisa Haki Afya wa Sikika, Bi. Geline Fuko akiwasilisha mada juu ya Katiba mpya kutambua haki ya afya na kuipa ulinzi katika mkutano wa vijana kutoka shule za sekondari na vyuo vikuu nchini.

Bi. Geline alisema Katiba mpya inatakiwa kuweka mifumo itakayofanikisha utawala bora katika sekta ya afya, kuimarisha uwazi na uwajibikaji. “Katiba itambue utawala wa sheria na pia itambue haki ya afya na haki ya kupata huduma za afya.” Alisema kwamba kuwepo kwa mfumo wa demokrasia kutatoa nafasi kwa watumiaji na watoa huduma kushiriki kikamilifu katika mipango na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za sekta ya afya nchini.

Afisa huyo alisema kwamba hali katika sekta ya afya nchini hairidhishi. Alitoa mifano ya ufuatiliaji na tafiti mbalimbali zilizofanywa na Sikika ambazo zilibaini upungufu wa bajeti, dawa na vifaa tiba, uhaba wa magari ya kusafirishia wagonjwa wakati wa dharura, upungufu wa rasilimali watu na ukikwaji wa maadili ya watoa huduma za afya; kama baadhi tu ya matatizo yanayoikabili sekta ya afya.

Wakichangia mada, washiriki wa mkutano huo walikiri uwepo wa huduma duni za afya nchini. Walilinganisha sekta ya afya wakati wa uhuru ambapo huduma za afya zilikuwa bure kwa wote na sasa ambapo wananchi wanachangia lakini hali inazidi kuwa mbaya.

Bi. Geline aliwataka vijana kushiriki kikamilifu katika mchakato wa katiba na hasa kwenye uchaguzi wa wawakilishi wa mabaraza ya Katiba na wakati wa kura za maoni.

Mkutano huo uliandaliwa na *Global Platform* kwa kushirikiana na *Action Aid Denmark.* Lengo lilikuwa ni kuwahamasisha vijana kushiriki kikamilifu katika mchakato wa kutengeneza katiba mpya.

Sikika

Nyumba Na. 69
Ada Estate, Kinondoni
Barabara ya Tunisia
Mtaa wa Waverley
S.L.P 12183
Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 26 663 55/57

Ujumbe mfupi: 0688493882
Faksi: +255 22 26 680 15
Barua pepe: info@sikika.or.tz
Tovuti: www.sikika.or.tz
Blog: www.sikika-tz.blogspot.com
Twitter: @sikika1
Facebook: Sikika Tanzania

Nyumba Na. 340
Mtaa wa Kilimani
S.L.P 1970
Dodoma, Tanzania
Simu: 026 23 21307
Faksi: 026 23 21316